**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 8 Septemba 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishekh
Ally Salum
Dominata Rwechunguiza
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassani Mibweto
Juma Imori Rugole
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Mejah Mbuya
Musa Athumani Lahi
Mussa Omari
Patrick Maziku
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali
Rashidi Saidi Karanji
Saimon Tobiasi
Shukuru Hassan
Sosthenes C Amlima
Yusufu Juma

**Msafara wa baiskeli**
Dominata, Paulo, Shukuru na Elaine waliandaa tangazo na Dominata aliwasiliana na vyombo vya habari kuwaalika kwenye mkutano wetu leo. Channel Ten na ITV walihudhuria mkutano na kutuhoji kuhusu msafara na kuchukua picha ya video tukiwa tumepanda baiskeli.

Mejah na Elaine waliarifu kuhusu mchakato wa kupata ufahdili. Ubalozi wa china ulitoa baikeli tatu kama zawadi za bahati na sibu na meja alizichukua na kuzipeleka nyumbani kwa Elaine. Zinahitaji kufanyiwa matengenezo kabla ya kutumika kwenye msafara Juma alipeleka barua ya kuwashukuru kwa mchango wao na kuwaalika kwenye msafara.

Tuliitwa kukutana na Ultimate Security, Elaine na Juma walikwenda jumanne. Walisema watatoa gari la wagonjwa na ulinzi kwa ajili ya msafara. Elaine aliwaomba kuchangia zawadi ya bahati na sibu na walisema wataongea na meneja wao kuhusu hili.

Elaine na Juma walikwenda Knight Support, Celtel na Game siku ya jumatatu. Knight Support, utawala haukuwepo. Tulikutana na Bibi Tuno ambaye ni mkuu wa ufadhili Celtel mwanzoni alionekana kuwa tayari kutusaidia lakini baadae alipiga simu na kusema mwamba celetel haitaeza kutoa ufadhili.

Game hawakupata barua yetu ya kwanza kwani ilipelekwa kwa makosa ofisi nyingine. Wakati Elaine alipopiga kufuatilia meneja utawala aliambiwa kwamba maamuzi yatatolewa na meneja was too ambaye yuko nnje ya nchi na atarudi mwishoni mwa Septemba.

Juma lipeleka barua kwa Mhe. Azzan Zungu kuomba kutumia, mahema, umeme na ukumbi katika Mnazi mmoja

Jumatatu Elaine na Juma walitoa Tsh 28,000 benki na kumpa Sosthenes. Sosthenes alitengeneza vibendera kwa ajili ya baiskeli za msafara ila hakuzileta kwenye mkutano hadi wiki ijayo.

Mejah alipendekeza kwamba tutengeneze bango kubwa kutangaza msafara na kuyaweka kando ya barabara ilikubalika kutengeneza mabango manne na ununuzi wa karatasi ilikadiriwa Tsh 55,000 ambayo itatolewa benki jumatatu.

Ilijadiliwa kwamba tunahitaji tiketi za bahati nasibu na bei itatafitiwa wiki hii.

Meja anavifaa vya muziki lakini hana uhakika ikiwa vina sauti ya kutosha hivyo ni bora / vizuri kupata kwa mtu mwingine kwa mfano Hussein Ali wa AALOCOM.

Elaine aliandika barua ya mwaliko na Juma alizipeleka kwenye chuo cha usafirishaji Dar es Salaam, Meya wa Temeke na Dar es Salaam, TANROADS< HUWATA na chama cha walemavu Tanzania (CHAWATA). Atapeleka barua zilizosalia SUMATRA, wizara ya miundombinu na meya wa kinondoni jumatatu. Ilikubalika kuandika barua DARCOBOA chama cha wamiliki wa mabasi kuwaalika.

Elaine alileta vipeperushi na mabango kwa ajili ya msafara kwa lugha za kiingereza na Kiswahili ilikublika kutengeneza vipeperuzi 200 kwa gharama za Tsh 30,000 na mabango 300 kwa Tsh 9,000. fedha hii itatolewa benki jumatatu na Shukuru atatoa nakala (urudufishaji)
Ilikubalika kwamb tukachukue maji ya kunywa kutoka kampuni ya Bakhresa na kuyahifadhi kwenye nyuma ya Elaine mpaka siku ya msafara.

**Ofisi**
Elaine aliongeza katiba kwenye ubao wa matangazo Ally Saidi Mohammedi alisema hakuwa na muda wa kurekebisha fremu na kutengeneza meza kama ilivyokubalika wiki iliyopita ila atatengeneza wiki ijayo. Mejah alisema atachora picha za baiskeli mlangoni mwa ofisi

**Guta**
Jumanne alileta Tsh 7,000 za mwendelezo wa malipo ya guta, jumla alisahau kitabu cha risiti hivyo malipo yaliahirishwa hadi wiki ijayo.

**TANROADS**
Juma alitembelea TANROADS na kuongea na mtu aitwaye isaak ambaye alisema majibu ya barua yetu bado hadi wiki ijayo alisema pia kwamba UWABA itatakiwa kuhudhuria tarehe 26 septemba kutoa mada. Wanachama walitakiwa kukumbuka tarehe hiyo.

**Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.**
Elaine alitembelea halimashauri ya jiji la Dar es Salaam, kitengo kinachoshughulikia usafirishaji walisema hawajaiona barua yetu ingawa tuiipeleka kwenye ofisi husika ya kupokea barua. Aliwapa nakala na walisema watajibu. Aliongea pia na mshauri wa kijapani wanaofanyia kazi mpango madhubuti wa usafirishaji Dar es Salaam, Junji shibata wa pacific Consultants International. Alisema tatizo kuu ni kwamba hapakuwa na barabara zilizobuniwa kwa Dar es Salaam Elaine alisisitiza uhitaji wa ushauri na wadau kama UWABA.

**Vitambulisho**
Elaine alileta vitambulisho ambavyo havijakamilika, baadhi ya wajumbe walisaini na kumpa Paulo Tsh 500 kwa ajili ya kukamilisha. Wengine waliomba vitambulisho vyenye muundo mpya.

**T- shirts**
Meja alisema kwamba amekutana na mtu ambaye atatoa tovuti bure w.w.w.uwaba.or.tz.ambayo itakuwa bora zaidi yah ii ya sasa w.w.w.geocities.com/ uwabadar.

**Kituo cha dala dala Mwenge**
Wanachama walisema kuna tatizo kwenye kituo cha mwenge ambapo upande mmoja wa geti wanaruhusu baiskeli kuingia lakini upande mwingine wanahusika wanawalipisha fine kwenye baiskeli kuingia ndani. Pia hakuna sehemu za kuegesha nje ya kituo. Ilikubalika kuandika barua halmashauri ya Kinondoni kutaka kujua sera inayohusika kituoni hapo.